# Kichaka

**Abubakar Nkundwason**

*Chapisho la kwanza; May, 2026.*

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inaruhusiwa kuhamishwa kwa namna yoyote ile, iwe ya kimaandishi au kielektroniki bila ridhaa ya maandishi kutoka kwa mwandishi. Kukiukwa kwa agizo hili ni uvunjwaji wa sheria.

*©MWANDISHI*
Abubakar Nkundwason

Msanifu kurasa: Diaro Alex
Mhariri: Joe Lwebagaramu.

Wasiliniana nami:
WhatsApp: +255 753 905 099
Kimechapishwa na: SAI Connection.
Dar es Salaam.

ISBN: 978-9912-43-678-3

# SHUKURANI

Shukurani zangu za dhati zimwendee Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na ardhi, kwa rehema, uhai na uwezo alionijalia mpaka kufanikisha kazi hii. Hakika bila yeye yote haya yasingewezekana.

Shukurani za pekee pia zimwendee baba yangu mzazi, marehemu Mzee Athuman Nkundwason Kimunason; Mungu amlaze mahali pema peponi. Baba yangu alikuwa sehemu muhimu ya msingi wa maisha yangu, na mema yake yataendelea kubaki moyoni mwangu siku zote.

Aidha, namshukuru mama yangu kipenzi, Hamida Mussa Rashid, kwa malezi yake, upendo wake, dua zake na moyo wake wa kujitoa ambao umekuwa faraja kubwa katika maisha yangu yote.

Shukurani za dhati pia kwa mke wangu mpendwa, Sumaiya Sandali Chowo. Hakika umekuwa nguzo imara katika maisha yangu, na uwepo wako umeendelea kunipa nguvu na faraja katika kila hatua ya safari hii.

Vilevile, shukurani zangu ziwaendee watoto wangu wapendwa: Sameer A. Nkundwason, Farheen A. Nkundwason, Adady A. Nkundwason pamoja na Amir A. Nkundwason. Upendo wao na uwepo wao ni sehemu ya furaha na hamasa katika maisha yangu.

Kwa wote waliokuwa sehemu ya safari hii kwa namna moja ama nyingine, Mwenyezi Mungu awalipe mema kwa wingi.

## DIBAJI

Fasihi ya Kiswahili imeendelea kukua kwa kasi kubwa, na ukuaji huo umechochewa na waandishi wanaothubutu kuibeba jamii yao na kuiweka ndani ya maandishi yanayogusa uhalisia wa maisha ya kila siku.

Miongoni mwa waandishi hao ni Abubakar Nkundwason, ambaye kupitia kazi hii ameonesha uwezo mkubwa wa kuchora picha halisi ya jamii yetu kwa jicho la ukosoaji, maonyo na tafakuri nzito juu ya mwenendo wa maisha ya mwanadamu wa leo.

Riwaya hii imebeba simulizi pana yenye kuakisi mapambano ya maisha, tamaa za binadamu, usaliti, rushwa, siasa, tamaa ya madaraka pamoja na mabadiliko ya tabia katika jamii. Mwandishi ametumia ustadi mkubwa wa lugha kuwasawiri wahusika wake kwa namna inayoifanya hadithi hii ionekane kana kwamba si simulizi la kubuni, bali ni taswira halisi ya maisha yanayoendelea mbele ya macho yetu kila siku.

Kupitia wahusika kama Seyunguson, Singasinga Mukesh, Mnyaru, Mtasha na wengineo, msomaji anapata nafasi ya kuitafakari jamii yake kwa kina. Kuna maswali mengi yanayoibuliwa ndani ya kazi hii kuhusu maadili, matumizi mabaya ya madaraka, tamaa ya utajiri wa haraka pamoja na namna ambavyo baadhi ya watu wameigeuza jamii kuwa sehemu ya kupigania masilahi binafsi pasipo kujali madhara kwa wengine.

Kilichonivutia zaidi katika kazi hii ni namna mwandishi alivyoimudu lugha ya Kiswahili cha Tanzania Bara kwa ufasaha mkubwa. Lugha iliyotumika ina mvuto wa kipekee, imejaa misemo, taswira, falsafa pamoja na mazungumzo yanayoipa riwaya hii uhalisia mkubwa. Aidha, mwandishi ameweza kuwajenga wahusika wake kwa umakini kiasi kwamba kila mmoja anaonekana kuwa na nafasi na mchango wake wa kipekee ndani ya simulizi hili.

Ni wazi kuwa mwandishi hakulenga kuburudisha pekee, bali pia kuifunza, kuiamsha na kuikumbusha jamii juu ya hatari ya kuhalalisha maovu, tamaa na kupotea kwa misingi ya utu. Hivyo, msomaji atakayepata nafasi ya kuisoma kazi hii atajikuta si tu akiburudika, bali pia akijifunza na kutafakari mambo mengi kuhusu maisha na jamii inayomzunguka.

Kwa msingi huo, ninaamini kuwa riwaya hii itakuwa miongoni mwa kazi zitakazopokelewa vizuri na wasomaji wa fasihi ya Kiswahili, hasa wale wanaopenda simulizi zenye uhalisia wa maisha ya jamii ya Kiafrika na hasa Tanzania ya leo.

Hongera kwa mwandishi kwa kazi hii nzuri na yenye mafunzo makubwa.

Joe Lwebagaramu
*Mhariri.*

*Mpaka simba watakapopata waandishi wao wenyewe,*
*hadithi za uwindaji zitaendelea kumsifu mwindaji.*

*— Methali ya Kiafrika*

## *Sura ya Kwanza*

*Sengeleni, Mingoni, 2017.*

### *Seyunguson; Zakayo Mtoza Ushuru*

Akrabu za saa zinakimbizana na kusakamana; huyo huyo, mkamate mkamate; kibarua ni pevu; lakini, pamoja na kuchacharika huko kote, hakuna akrabu inayofua dafu hata kumkamata mwenzake.

Kila iliyokuwa mbele haitaki kupitwa. Inajitahidi kwa kila hali kuwa kinara, mwishowe, hatima ya vishindo na kasi yake; saa zinaonekana kwenda msobesobe.

Liamba umefumbua macho hujatahamaki machwa haya hapa. Siku, juma, mwezi na mwaka tena si kitu. Vinavyopita utasema havikuwahi kuwepo. Leo imefika, jana inabaki historia. Na ukiitazama jana, unaiona imepita haraka mno. Ukiwa bado kinywa wazi, unatafakari leo imefikaje; kesho nayo inaingia punde kwa kishindo chake.

Ni kana kwamba, hizi siku zinashindana, zinavutana na kupigana vikumbo; itoke hii iingie nyingine. Na hiyo inayoingia haikai kitako. Itasongwasongwa na kusukumwa, mwishowe itakiacha kiti na kuipisha nyingine tena; hali hiyo imepelekea, baadhi ya waja wamepoteza stahamala maana siku zapita kasi, lakini hali zao za kimaisha zipo palepale.

Waja hao, waliitumainia kesho. Ila kesho wapi! Kesho ndiyo hiyo jana na leo, zilizopita mfano wa upepo. Wamefika mahala, wanaona matumaini yao wasiyaweke tena kwenye siku. Lakini, wayaweke wapi? Kwenye yale waliyonayo? *Mh!* Wanayapi sasa hata wajivunie na kuweka matumaini kwayo? Wamegeuza macho, wamekosa sehemu ya kutazama sasa wanageuza mawazo; Wanaona heri wale walionao! Lakini, mawazo hayo yanachochea tu jaka la moyo! Hayana majibu shadidi. Wale walionao, si ndio hao wanaopukutika kila uchwao mfano wa majani makavu ya mti wakati wa kiangazi? Ukifikiria ni kana kwamba, siku zinaingia na kuondoka nao! Hakika, hawana mahala pa kupetukia hata waseme kuna unafuu!

Seyunguson, ni miongoni mwa waja waliopoteza stahamala. Wale ambao mbio za akrabu za saa zinazounda siku, ziliwasababishia ndwele mioyoni mwao. Wakipima waliyoyafanya huko muda utokako na hapa ulipowafikisha – wanajihesabu ni fungu la kukosa. Kilichowaumiza zaidi ni dalili wanazoziona kuwa; huenda muda utawaacha wakiwa hivyohivyo walivyo – wakata – hohehahe wasio na kitu!

Hata hivyo; hahati inamuujiza wake ingawa haina ahadi. Tofauti na siku nyingine; leo, Seyunguson, moyo wake umefurika matumaini kiasi ameshindwa kuyazuia yasimwagike nje. Huyo, katoka atokako kachapa mguu mpaka kwa chanda chake, yule mja wa kufa na kuzikana naye – yule waliyesemezana ya kuyasema hata wasiyamalize. Msiri wake na kimbilio kwenye shida zake; Bwana aitwaye Ntakebukason. Walipokutana, akamuweka kitako baoni, nje ya nyumba yake na kuunadi mchapo uliomtembeza maili zote hizo alizokanyaga atokako.

Bwana Ntakebukason alimuofa rafiki yake bia ili amtapikie

yote aliyonayo moyoni.

“Sasa nimefikiwa!” Seyunguson alitamba akichanua tabasamu la haja. Meno yote ameyaanika nje angali hakuna jua la kuyakausha. Bwana Ntakebukason alimdadisi;

“Umefikiwa na nini?”

“Namaanisha muda wangu wa kutoka umefika.”

“Kutoka kwenda wapi?”

“Bwana wewe, muda wangu wa kutoboa...”

“Kutoboa nini?”

“Ebo!”

“Sikuelewi ati!”

“Wacha kujitia uzuzu bwana!”

“Wala si uzuzu. Hueleweki! Mara umefikiwa, mara utoke, mara utoboe – wazungumzia nini haswa?”

“Namaanisha, mlangoni kwangu ukabwela umefika kitembo.”

“Kwamba unaelekea kuwa bwanyenye?”

“Haswaa! Hapo zimekurudi kichwani!”

“Ha! Ha! Haaaaa!” Bwana Ntakebukason alivunjika kwa kicheko, almanusura achane mbavu zake, “hebu niache bwana, usianze kunichekesha ovyo utasema nina raha za maisha … kwa dili lipi ulilokutana nalo mwenzetu mpaka uwe bwanyenye?”

“Tatizo unanichukulia wa viwango vyako. Unaniona mie sawa na wewe hohehahe wa mwisho! Mwaka umeenda mwaka umerudi upo palepale, mwenzako nishakuwa mtu wa maana kabisa. Punde utatubu mbele zangu.”

“Wewe bwana acha kuota ukiwa macho wazi…” Ntakebukason alisema na kuendelea kucheka, “hahahaaaa!”

Bwana Seyunguson alimtupia Ntakebukason jicho kavu, kisha akasukuma kite kana kwamba anafadhaika. Ndipo

akamwambia: “Cheka taratibu usije ukaachia mashuzi.”

“He! hee!” Ntakebukason, aliendelea kuvunjika kwa kicheko. Huyu rafiki yake, leo anamuona amepania kumvunja mbavu. Amegeuka onyesho la bure la visa na mikasa ya kuchekesha.

Ati atoke kimaisha na kuwa bwanyenye! Seyunguson huyu huyu anayemjua? Kilikuwa ni kituko cha mwaka.

Bwana Ntakebukason, baada ya kucheka tani yake, hatimaye alimwambia Seyunguson, “ Na bora tu hayo mashuzi yanitoke. Si kwa habari hizi za leo. Ama hizi bia tunazokunywa zimeongezwa kiwango cha ulevi!”

Khm! Bwana Seyunguson alijikuta akibwaga mguno, naye akaishia kucheka kutokana na namna ambavyo huyo mwenzake, Ntakebukason alivyokuwa anazidi kuvunjika kwa kicheko, kutokana na habari zile alizompa. Kwamba, uchochole wake unaelekea kitembo na umefika muda wake wa kuhama daraja. Kwa mipango aliyonayo, anaona wazi, hata wanga, washirikina na sangoma wote wa kijiji hicho cha Sengeleni waungane, hawawezi kumrudisha nyuma. Wakati wake wa kukaa meza moja na wakwasi umewadia. Naye akiwa mmoja kati ya hao wenye misuli na sauti ya fedha.

“Una dili gani mwenzetu, hebu nipe za nyuma ya pazia pengine nitakuelewa unachojaribu kuniambia…”

Seyunguson aliokota mezani chupa yake ya bia na kuipandisha mdomoni. Kisha alimimina bia hiyo mdomoni kama maji. Akakunja sura wakati akiilazimisha ipite kooni, ndipo akashusha chupa mezani. Ulisikika mshindo wa haja wakati akiitua chupa ile ya bia.

“Ah! Wewe siunamadharau… subiri ujionee kwa macho!”

“Bwana, hebu tuache masihara. Sasa nimekuwa makini, nielekeze…imekuwaje?”

“Hufahamu nakula na wakubwa?”

“Mkh!” Ntakebukason aliguna,“Seyunguson... Seyunguson acha maneno mengi… yani hao wakubwa wakose watu wa kula nao wale na wewe?”

“Dharau zako mbona zitafika kitembo, tuombe tu heri utajionea kwa macho yako ya nyama!”

“Bwana wewe wacha majigambo. Ikiwa ulishindwa kutoboa kwenye ujana wako usitegemee sasa; tunu yako imekwisha pita. Umebaki unajisumbua na mawazo yasiyo na uhalisia. Kwa kazi gani tunayofanya hata utoboe? Au hizo chauchau unazosotea kwa wafanyabiashara wa Soko Maziwa ndizo unafikiri zitakutoa kwenye ukabwela?

“Huko ni kujidanganya ndugu yangu. Ama ukizidisha, ukazifakamia kwa tamaa, utakuwa unatafuta sababu ya kuozea jela hivyo!”

Bwana Seyunguson, aliishia kubwaga pumzi ndefu. Huuuuu! Uso ukamshuka. Mchapo uliomtembeza himahima kuja kumweleza huyu rafiki yake umegeuka fimbo ya kumchapia. Utasema Bwana Ntakebukason, ambaye ni rafiki yake mpendwa, alimpania siku hiyo. Kisebusebu chote kilichomtoa atokako kilimwisha.

Hata hivyo, pamoja na maneno ya kejeli ya rafiki yake, picha aliyonayo Seyunguson akilini mwake, ni ya Mafanikio makubwa, aliyokuwa anayaona mbele yake. Kutokana na kejeli hizo, alitamani kungekuwa na uwezekano wa yeye kufanya miujiza, angefanya, ili amthibitishie huyu rafikiye juu ya hilo. Lakini, uwezo wa kufanya miujiza hana. Na wala, hana namna ya kusema anaweza kuichapa picha ya yale anayoyaona akilini mwake, hata mwenzake aweze kuiona na kusadiki. Inambidi tu, awe mpole!

“Tunywe bia zetu bwana. Achana na hizo habari. Na kama

umekwisha lewa basi twende'zetu tukapumzike na wake zetu!" Bwana Ntakebukason, alimwambia Seyunguson akizoa chupa yake ya bia mezani na kubugia funda kadhaa.

*****

Seyunguson ni jina lililofahamika katika kijiji cha Sengeleni hapo mjini Mingoni. Ni jina la babu yake, lakini lilimtambulisha kuliko majina yake mawili ya awali.

Kuanzia akiwa kinda hata sasa ni shababi jitu la miraba minne. Wengine wanamuita mkongwe, kutokana na nywele nyeupe kuanza kuchipua kichwani na kwenye masharafa yake, zikiwa ni kiashiria kuwa umri umeanza kumtupa mkono; Seyunguson alifahamika kwa jina hilo.

Hata hivyo, hilo la umri kumtupa mkono lituweke kitako kwa sekunde chache. Hilo lilikuwa ni jinamizi linalotisha mbele ya bwana huyu Seyunguson. Kila mara lilipomtokea liliichachafya nafsi yake. Akifikiria juu ya umri wake na kuuzidisha mara mbili, jawabu lake lilimkosesha amani.

Aliona tayari muda umekwisha mtupa mkono hasa alipojilinganisha umri wake na watu anaowafahamu wenye umri wa kulandana naye.

Nafasi aliyonayo kwenye maisha ilimfanya Seyunguson ajione ni mtu wa mwisho kati ya watu wote duniani.

Zuzu! Kuna wakati alijihesabu hivyo. Alijihesabu yeye kuwepo katika nafasi hiyo ya maisha kumetokana na ubahau wake ama tuseme, ulimbukeni pamoja na ushamba.

Hayo yote aliyoyadhani, ndiyo haswa yamechangia kumfanya awe mahala hapo. Akiyajumlisha kwa pamoja anajiona yeye ni zuzu kinara kati ya mazuzu wote waliopata kutokea kwenye ulimwengu huu!

Eti leo anaishi kwa kusota? Maisha ya 'jana ni nzuri kuliko leo!' Kuna muda bwana Seyunguson, alikuwa akihisi kwamba yupo ndotoni na kuna siku ataamka na kukuta anaishi maisha yake, maana haya anayoishi anayahesabu wazi si maisha yake! Anahisi pia, huenda kuna watu walimchezea kichwa na kumpora nyota kisha wakamtumia jini la chuma ulete, maana si bure! Anaona jini hilo limechuma kila kitu na kumuacha hivyo alivyo sasa.

Kwa kuzaliwa, Seyunguson alichomoza toka tumboni mwa mama yake akiwa na nyota yake timamu. Nyota ya kuvuma. Kusifika. Kuishi midomoni mwa watu. Kwa mema alitambulika na kwa mabaya alijulikana. Hayo yote yalimfanya Seyunguson kuwa Seyunguson. Alinuka umaarufu. Hapakutokea mahali hapo Mingoni, jina lake halikufika.

Toka ni kijana barobaro aliyewachengua warembo. Toka akiwa mwembamba hajapata mwili kama alionao sasa, ambao humfanya wengine wamuite pipa au kibakuli, kutokana na alivyonenepeana, kimo chake kikiwa kifupi na tumbo likitangulia mbele atembeapo na kiwiliwili kikifuata nyuma;

Toka akisakata soka na kusifika. Sifa zilizovuma mitaani, zikapanda wilayani na kuenea hata mkoani.

Zikampandisha daraja, akazitimba nyasi za viwanja vyote vikubwa vya Mingoni. Soka likamuheshimisha na kumpa chati. Halmashauri ya mji huo ikamuona. Ikahitaji huduma yake kwenye timu yake ya soka ya halmashauri ya Mingoni, wakamnasa na kumpatia ajira.

Seyunguson kwa kipawa chake akachanua mfano wa ua waridi katika liamba pevu. Watoto wakaliimba jina lake: *'Seyunguson na mpira, Seyunguson na mpira, kashuti gooooo!'* Seyunguson alikuwa ni maana halisi ya utamu kwenye mchezo huo wa soka na kipawa chake kiliitafsiri raha ya wapenzi wa

soka wa timu aliyochezea. Kupitia umahili wake, timu yake nayo ilisifika pamoja naye na ilivuna mashabiki lukuki.

Hata hivyo; Waswahili wanamisemo yao bwana juu ya daraja hili la mafanikio! Utasikia: fanikiwa tuifahamu tabia yako! Wengine watakwambia; mafanikio yanalevya! Basi, hayo ya Seyunguson ukiwa huyafahamu unaweza kudhani hizo ni porojo za wahenga. Lakini, kila mwenye sikio aliyepata kusikia, na mwenye macho aliyepata kuona, kathibitisha mwenyewe kwamba, hizo zilikuwa ni busara. Na wehenga, kama si yote basi walifahamu mengi; na hata hili walilifahamu kwa mapana yake. Hili la; fanikiwa tuifahamu tabia yako!

Wengine walisema: masikini akipata matako hulia mbwata! Hayo ndiyo yakawa ya Seyunguson sasa. Zile sifa na kuvuma kwake vilimlevya. Akafika mahala pa kujiona yeye ndiye yeye na hakuna mwengine aliyebarikiwa zaidi yake hapo Mingoni. Huo mtazamo ukamfanya ajawe na kiburi, jeuri na ubahaluli. Hatimaye, sifa hizo zilizomvumisha na kumpaisha zikageuka sifa za mgema. Zikamfanya alewe yale mafanikio aliyokuwa nayo. Basi tuwi akalitia maji!

Seyunguson alikuwa na matumizi mabaya ya pesa. Alipomaliza kuhenyeka uwanjani na kuzinasa pesa zake mkononi; alizitawanya kwa kustarehe na warembo wa kila aina tena kwenye kumbi mbalimbali za starehe za mji huo.

Akajulikana kwenye kumbi hizo sawa na alivyojulikana kwa mashabiki wa soka awapo dimbani. Vijana wakambatiza jina; Mzee wa kujimaliza! Kutokana na makeke yake akiwa baa. Kiasi cha pesa alichokwenda nacho baa, Seyunguson alihakikisha kinaisha ndiyo angefahamu mlango wa kutokea upo mahala gani.

Kutokana na hayo yote, imefika hatua akatelekeza familia yake. Akawa ni mtu wa kuoa na kuacha. Mwezi Mtukufu

wa Ramadhani ulipogonga hodi; Seyunguson alikuwa ni mtakatifu hapakutokea kama yeye. Kanzu mwilini, baragashia kichwani na makubazi mguuni. Mkononi hakukosa tasbihi na uchebe wake ulioga hina ndembwendembwe! Sheria za dini alizishikia bango, akawasakama mashekhe na maimamu wamuozeshe atimize suna yake ya dini.

Mwezi huo mtukufu ulipotokomea, naye alitokomea kwa kutelekeza mke. Ndoa akaipa kisogo. Basi sasa, hayo yote yakaungana na yale wahenga waliyosema; 'mshika mawili moja humponyoka!' Starehe zilipomteka Seyunguson soka lilimshinda!

Hatimaye akiwekwa uwanjani akawa anarukaruka tu; hajulikani anacheza nini – singeli si singeli, makida si makida, basi tu kiwango chake kiliporomoka kwa kasi mno. Mwishowe, akiwa bado kijana ambaye alikuwa anatazamwa na wapenzi wa soka wa Mingoni, kwamba atafika mbali katika mchezo huo, kupita wanasoka wote waliowahi kupata kutokea katika mji huo, alitemwa na timu yake na hapakuwa na timu iliyomhitaji. Ama kweli; matarajio si mapato. Ndoto za watu wengi ziligeuka kuwa ndoto za Ali Nacha. Seyunguson naye baada ya kuona amepoteza utukufu wake katika soka aliamua kubaki na kofia moja. Kofia ya ajira. Akabaki kuitumikia halmashauri kupitia kwenye kitengo cha utozaji ushuru. Ambapo, alipangiwa kituo cha kazi katika kijiji cha Sengeleni huko alikokutana na Bwana Ntakebukason.

Naye huyu bwana kwakuwa alizaliwa na nyota yake ya kuvuma – huko nako masokoni alikotoza ushuru alivuma haswa; huko alibatizwa jina la Zakayo mtoza ushuru.

*Mapinduzi ya kweli hayawezi kuanza barabarani,*
*yanaanza ndani ya fikra zako.*

## *Sura ya Pili*

*Vita vya Nzige*

Siku hazifanani. Wala hazilingani. Siku hutofautiana. Kwa mengi; kwa maringo na vituko vyake, ama kwa fujo na uraufu wake. Kuna siku za nakama, furaha na huzuni; zote hizi ni siku katika maisha ya mwanadamu.

Hiyo siku, ambayo Seyunguson alikuwa anazungumza hayo ya kuuaga ukabwela, ilikuwa ni kati ya zile siku za furaha kwake, maana ilianza kwa kicheko na ikatamatika kwa kicheko, ndiyo maana pengine, alipata hayo ya kumweleza chanda wake Ntakebukason.

Siku hiyo, pamoja na kwamba, ilianza kama siku nyingine za juma; ikiwa na hali ya hewa ya kupoa angani, baadaye jua lilipoamka na kuchachamaa, ilichangamka na kuwakarahisha baadhi ya waja.

Liamba ilipowadia, kabla Seyungusonhajashusha mguu wake kitandani, alipata simu kutoka kwa bwana mmoja singasinga aitwaye Mukesh Baltazar. Ambaye ni mfanyabiashara mwenye heshima na utukufu wake, hapo Sengeleni katika eneo la Soko Maziwa.

Bwana huyu Mukesh, alikuwa anafanya biashara za kuuza vitambaa mbalimbali vya kushonea mavazi alivyovitoa huko Asia; alikuwa na biashara za vifaa vya ujenzi, alimiliki pia bakery, pamoja na migahawa!

Simu kutoka kwa Mukesh, ilikuwa ya heri kwa Seyunguson. Kuanza siku na simu hiyo, ni kwamba; Mwenyezi Mungu aliamua kumkirimia siku hiyo, maana alifahamu hawezi kwenda kwa huyo bwana, na kwa ukwasi alionao, atoke mikono nyuma, kichwa chini. Alifahamu, ni lazima atapata posho ya kumfanya ashinde anachekacheka siku nzima, utasema mwendawazimu kaona jalala jipya.

Seyunguson, baada ya kutoka bafuni aliulamba mkanda nje. Kwa dakika kadhaa alitulia mbele ya kioo akachana nywele na kuyaweka sawa masharafa yake, ndipo akatoka. Alipofika ofisini kwa Singasinga Mukesh, alikaribishwa kwenye kiti cha magurudumu, kilichokuwa mbele ya meza kubwa iliyobeba makarabrasha mengi. Singasinga Mukesh, yeye alikaa upande wa pili wa meza ile, kwenye kiti cha magurudumu kilichofanana sawasawa na hicho alichokuwa ameketi Seyunguson.

Tofauti na siku zote, ambazo Seyunguson amewahi kutembelea ofisini hapo, siku hiyo alipokelewa mapokezi ya kifalme. Kupewa ofa ya alikasus na kashata na Singasinga huyo, mwenye madharau na jeuri ya pesa, kwa Seyunguson lilikuwa ni jambo la kuheshimiwa mno.

Baada ya mazungumzo ya hapa na pale, wakiyasukuma mazungumzo hayo na alkasus pamoja na vitafunwa, Singasinga Mukesh alimwambia bwana Seyunguson:

"Muda wako wa kuuaga uchochole umewadia!" Alisema akitabasamu.

Maneno hayo yaliufanya moyo wa Seyunguson ubadilishe

mapigo yake kabisa. Ukaanza kwenda hobelahobela, utasema jiwe limerushwa kutoka juu ya mlima. Kihoro kimemjaa kwelikweli. Anajiuliza ni dili gani hili analamba asubuhi namna hii, la kumtoa kwenye uchochole.

Hakika hii siku imekuwa nyemi mapema mno!

"Sikiliza Seyunguson!" Yule Singasinga alimweleza. Seyunguson alishusha pumzi fupi na kukaa vyema kwenye kile kiti cha magurudumu ili aweze kusikia mpango ama dili hilo la kumtoa kwenye ufukara.

"Nina maadui kwenye biashara zangu hapa Soko Maziwa. Bila kuwashughulikia, nitaendelea kukimbia mbio za mende sakafuni. Kuna watu wawili nahitaji wanipishe kabisa barabarani!"

*Eh!*

Seyunguson sasa kinywa kimembaki wazi. Kile alichotegemea sicho anachokisikia. Kushughulikia watu? Kha! Akili na mwili vilichoka. Akajiuliza; *nawashughulikia kivipi?* Majibu hakuyapata haraka. Ikabidi alazimishe mate kumpita kooni.

"Sijakuelewa Singasinga! Unamaanisha nini?" Alijikakamua na kuuliza.

"Hilo swali ndilo nilikuwa nalitaka sasa." Mukesh alizungumza kwa kujiamini akizunguka zunguka kwenye kiti kile cha magurudumu.

"Hawa watu wamekwepa kodi kwa muda mrefu," alisema kwa msisitizo akiinuka na kukaa sawa kitini pale, "wanatumia njia za panya kuendesha biashara zao. Sawa, wote tunafanya hivyo, lakini hawa wamezidi. Sasa nataka utafute ushahidi wa madeni yao huko kwenye shirika la mapato. Nafahamu pia, huko unawatu unaweza kushirikiana nao kuwakaanga.

Mimi nitahakikisha nawawezesha kwa kila mnachokitaka,

ilimradi tu hawa watu watoke njiani."

Sasa, Seyunguson alilielewa jambo ambalo bwana huyu alikuwa akilimaanisha. Mambo ya fitina za namna hii kwenye biashara, Seyunguson anayafahamu vilivyo. Anafahamu wafanyabiashara wengi hufanyiana mambo hayo, naye ameshiriki kuangamiza watu wengi akitumiwa na watu ambao walimtunuku fedha baada ya kufanya hivyo. Moyoni mwake akajisemea; vita vya nzige hivi. Akili yake ilimweleza, huo ni wakati wake wa kunufaika mfano wa kunguru wanufaikavyo katika vita vya nzige. Akiwaza hayo, mwishowe alimuuliza Singasinga Mukesh: "Watu wenyewe ni kina nani?"

"Yule Mnyaru wa pale karibu na stendi ya mabasi, mwenye biashara ya vifungashio, duka la vifaa vya ujenzi na duka la dawa baridi. Pamoja na Mtasha, yule wa jirani yake, mwenye maduka pia ya vifaa vya ujenzi na urembo. Hawa watu wananinyima usingizi siyo siri. Ukiweza kutumia ujagina wako kuangusha biashara zao, hakika utanikumbuka daima dawamu.

"Nitakubadilishia maisha hutaamini kwa macho yako ya nyama. Kwani unahitaji shilingi ngapi kuanzisha biashara yako ya kueleweka Seyunguson? Sishindwi kukupa hata milioni kumi. Hizo kwangu ni pesa za madafu nawe nafahamu kwako si haba ati!"

Seyunguson, alijikuta akilazimisha mate ya baridi yaliyomjaa mdomoni kupita kooni. Pamoja na hayo majina aliyoelezwa kuyafahamu vizuri, akifahamu juu ya utata wa watu hao, pamoja na marafiki walionao serikalini na kwenye mashirika muhimu, lakini pesa alizotajiwa zilimtoa mate mdomoni.

Milioni kumi! Hakika ni pesa nyingi. Kwa kitendo cha haraka Seyunguson alijaribu kupiga hesabu zake kichwani, akazigawa pesa hizo kwenye mafungu kadhaa – fungu hili